



Haki ya Afya Tanzania

Uchambuzi wa Sikika

Uchambuzi wa Sikika kuhusu Rasimu ya Pili ya Katiba mpya. Waraka huu unawasilisha maoni ya Sikika juu ya vipengele vya sheria vilivyomo na visivyokuwemo kuhusiana na haki ya afya. Tunawakaribisha wadau wote kuunga mkono mchakato huu katika kushauriana na kujadili.

CHANGAMOTO AMBAZO HAZIJATATULIWA KATIKA MFUMO WA AFYA

Kwa miaka mingi, Tanzania imekuwa ni nchi inayoonesha ukuaji endelevu wa kiuchumi. Pamoja na ongezeko la ukusanyaji wa kodi, serikali ya Tanzania bado inapambana kuhakikisha usawa katika uwepo na upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote.

Mpaka sasa bado hakuna uwiano sawia wa vituo vya kutolea huduma za afya na idadi ya watumia huduma kati ya wilaya na wilaya. Mathalani, idadi ya vituo vya huduma za afya katika halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga ni mara kumi zaidi ya vituo vilivyopo katika halmashauri ya wilaya ya Geita. Kama kungekuwa na mgawanyo sawia, basi halmashauri ya wilaya ya Geita ingekuwa na vituo vya huduma 128 kwa ajili ya kuhudumia wananchi wapatao 850, 000 badala ya vituo 54 tu vilivyopo sasa. Kinyume chake, halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga yenye idadi ndogo ya watu wapatao 200,000 ina vituo vya huduma za afya 123 badala ya vituo 31.¹

Mbali na hayo, Tanzania bado inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa afya. Kwa mwaka 2012, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliripoti uwepo wa watumishi wa afya 64,500 tu ikiwa ni pungufu ya watumishi 133,000 ambao walihitajika kuhudumia wananchi zaidi ya milioni 43.² Hali hii imechangiwa zaidi na ukweli kwamba madaktari wengi (69%) hufanya kazi katika maeneo ya mijini wakati watanzania wengi (74%) wanaishi maeneo ya vijijini.³

Tanzania imekuwa ikikabiliwa na uhaba wa mara kwa mara wa dawa muhimu mathalani dawa za kutuliza maumivu naantibaiotiki katika vituo vingi vya huduma za afya vya umma. Matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2012 (The Tanzania Service Availability and Readiness Assessment (SARA)) yanaonyesha kuwepo kwa uhaba wa dawa muhimu kwa 63%.⁴ ambao husababisha wananchi wengi kuondoka katika vituo vya huduma pasipo kupatiwa matibabu sahihi.

¹ Ifakara Health Institute and Ministry of Health and Social Welfare (2013), Tanzania Service Availability and Readiness Assessment 2012, uk. 7.

² Ministry of Finance and Economic Affairs (2013), Volume II Public Expenditure Estimates Supply Votes (Ministerial) as Passed by the National Assembly 2013-2014.

³ National Bureau of Statistics (2011), Tanzania Demographic Health Survey (2010), uk. 12.

⁴ Ifakara Health Institute and Ministry of Health and Social Welfare (2013), Tanzania Service Availability and Readiness Assessment 2012, uk. 24, 27.

Tatizo hili sugu la uhaba wa dawa halitokwishampaka serikali itakapotenga fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa dawa zinazohitajika. Kwa mwaka huu wa fedha 2013/14, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imetenga shilingi za Tanzania bilioni 30.8 za mapato ya ndani kwa ajili ya ununuzi wa dawa muhimu na vifaa tiba. Wahisani wanachangia shilingi za Tanzania bilioni 28.5.⁵ Kiasi hiki cha fedha ni pungufu ya shilingi bilioni 140.7 ya mahitaji ambayo yanakadirwa kufikia shilingi bilioni 200. Pamoja na pengo hili la fedha, bado Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na idara zake, zimepanga kutumia shilingi bilioni 346.7 kwa ajili ya malipo ya posho, ambayo wananchi huchukulia kama matumizi yasiyo ya lazima yanayozua maswali juu ya umuhimu wake kwa ustawi wa wananchi.⁶

Zaidi ya hayo, vituo vingi vya huduma za afya havijaandaliwa vizuri kwa ajili ya kutoa huduma za afya ya msingi. Ili kupunguza kasi ya vifo vya mama na watoto wachanga kufikia watoto 454 kati ya 100,000 wanaozaliwa wakiwa hai, wamama wajawazito wanahitaji kufika katika vituo vya huduma za afya ambavyo vina watoa huduma wenye ujuzi, dawa na vifaa tiba maalum. Kutokana na utafiti wa SARA wa 2012, asilimia 74 ya vituo vya huduma za afya vya umma hutoa huduma za uzazi, lakini vituo hivyo vina upungufu wa zaidi ya nusu (51%) ya mahitaji muhimu kwa ajili ya huduma za msingi za uzazi.⁷

Kuna changamoto nyingine nyingi ambazo zinakwamisha wananchi kuweza kufurahia huduma bora za afya. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa Afya na Idadi ya Watu Tanzania wa mwaka 2010 (The Tanzanian Demographic and Health Survey, 2010) ambapo wanawake waliulizwa kuhusu matatizo wanayokumbana nayo katika kutafuta huduma za afya,⁸ takribani asilimia 24 walitaja upatikanaji wa fedha kuwa ni tatizo kubwa, 19% walilalamikia umbali wa vituo vya kutolea huduma za afya, huku asilimia 11 wakihofu kwenda peke yao katika vituo vya huduma. Mara nyingi matatizo haya huripotiwa na wanawake masikini, wanaoishi vijijini, wanawake wazee, wanawake wasio na elimu pamoja na wanawake waliotalikiwa, kutengana na waume zao ama wajane. Hivyo, kuna ushahidi mkubwa kuwa upatikanaji wa huduma za afya unahusiana na mambo mengine mbalimbali ya kijamii.⁹

Mwisho, ni marachache wananchi hushirikishwa katika masuala yanayohusu afya. Serikali inatambua ushiriki wa jamii na umiliki kama sehemu ya utoaji wa huduma za afya ya msingi zinazolenga mahitaji ya eneo husika.¹⁰ Lakini Sikika imebaini kuwa mbili ya tatu ya kamati za kudhibiti UKIMWI hazifanyi mikutano ya kisheria ya kila mwezi kama inavyotakiwa pia hazitoi mrejesho wa mipango na bajeti kwa jamii zinazoziwakilisha.¹¹

⁵ Ministry of Health and Social Welfare (2013), Medium Term Expenditure Framework for FY 2013/14-2017/18, uk. 14, 30.

⁶ Ministry of Finance and Economic Affairs (2013), Volume II Public Expenditure Estimates Supply Votes (Ministerial) as Passed by the National Assembly 2013-2014.

⁷ National Bureau of Statistics (2011), Tanzania Demographic and Health Survey (2010), uk. 141.

⁸ Ifakara Health Institute and Ministry of Health and Social Welfare (2013), Tanzania Service Availability and Readiness Assessment 2012, uk. 24, 27.

⁹ National Bureau of Statistics (2011), Tanzania Demographic and Health Survey (2010), uk. 141.

¹⁰ Ministry of Health and Social Welfare (2008), Health Sector Strategic Plan III, uk. 7.

¹¹ Sikika (2012), Multi-Sectoral AIDS Committees in Tanzania – A Gateway for Citizens' Participation.

HAKI YA AFYA KWENYE KATIBA YA SASA

Katiba inayotumika sasa haiwapi wananchi uhakika wa kisheria wa mahitaji muhimu ili waishi maisha yenye afya bora. Sehemu ya pili ya sheria kuu inataja malengo na miongozo muhimu ya sera za nchi:

11. (1) Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu, na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi. Na bila kuathiri haki hizo, Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anaishi kwa jasho lake.

Wakati serikali ilipaswa kutambua na kutumia malengo na maelekezo hayo, ibara ya 7 (2) inasababisha ibara zilizopo kuwa butu kwa kuzuia utekelezaji na usimamizi wake katika mahakama.

7 (2) Masharti ya Sehemu hii ya Sura hii hayatatiliwa nguvu ya kisheria na mahakama yoyote. Mahakama yoyote nchini haitakuwa na uwezo wa kuamua juu ya suala kama kutenda au kukosa kutenda jambo kwa mtu au mahakama yoyote, au kama sheria, au hukumu yoyote, inaambatana na masharti ya Sehemu hii ya Sura hii.

Matokeo yake, wananchi wanakosa njia madhubuti ya utetezi endapo haki ya afya haijapatikana.

HAKI YA AFYA KWENYE RASIMU YA KATIBA MPYA

Rasimu ya katiba haitoi maana iliyo wazi ya haki ya afya kwa wote. Hata hivyo, kuna vipengele vinavyohusiana na maswala ya afya.

- 41. - (1) Kila mtu anayeishi katika Jamhuri ya Muungano ana haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya.*
- (2) Haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya inahusisha haki kwa kila raia kutumia maeneo ya umma au sehemu mbalimbali za mazingira yaliyotengwa kwa madhumuni ya burudani, elimu, afya, ibada, utamaduni na shughuli za kiuchumi.*
- (3) Mtu yeyote anayeishi Tanzania anao wajibu wa kutunza na kuendeleza mazingira na kutoa taarifa kwa mamlaka za nchi kuhusu shughuli au jambo lolote ambalo ni hatarishi au lina uwezekano mkubwa wa kuharibu au kuathiri mazingira.*

Mazingira safi na salama ni kigezo muhimu ili watu waishi maisha bora na ya afya. Lakini kuna mambo mengine yenye athari kwa afya, kama mazingira ya kazi, maji safi na salama, lishe bora, malazi salama, usalama wa jamii kama watu hawawezi kujitunza na huduma ya afya ya msingi.

Kati ya haya, mahitaji matatu; lische, malazi na huduma ya afya zimeainishwa katika ibara ya 42 (1) (e) kama haki za mtoto.

43. - (1) Kila mtoto ana haki ya-

- (a) Kupewa jina na uraia;
- (b) Kutoa mawazo, kusikilizwa na kulindwa dhidi ya uonevu, ukatili na udhalilishaji;
- (c) kucheza na kupata elimu;
- (d) kuhifadhiwa katika mazingira mazuri, kwa walio katika ukinzani na sheria;
- (e) kupata lische bora, makazi na huduma ya afya;
- (f) Kushiriki katika shughuli zinazolingana na umri alionao; na
- (g) kupata malezi na ulinzi wa wazazi, walezi au mamlaka ya nchi, bila ya ubaguzi wa rangi, utaiifa, lugha, mtazamo wa kisiasa, jamii anayotokea, mali, uzazi, kabila, dini, jinsi au aina nyingine za hadhi.

Zaidi ya hayo, ibara 47 (1) (g) inawapatia wanawake haki ya huduma ya afya

47. - (1) Kila mwanamke ana haki ya:

- (a) Kuheshimiwa utu wake;
- (b) Kuwa salama dhidi ya unyonyaji na ukatili;
- (c) Kushiriki bila ya ubaguzi katika chaguzi na ngazi zote za maamuzi;
- (d) Kupata ujira sawa na mwanaume katika kazi;
- (e) Kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu na mila zenye madhara;
- (f) Kulindwa kwa ajira yake wakati wa ujauzito na pale anapojifungua; na
- (g) Kupata huduma bora ya afya inayopatikana.

Wakati huduma ya afya ikiwa ni muhimu kwa watoto na wanawake wote, kuna makundi mengine yenye mahitaji maalum ikijumuisha wazee, watu wenye ulemavuwa mwili, wagonjwa waakili nawengine wenye mahitaji muhimu yanayotakiwa kutolewa na mfumo wa afya wa taifa.

Kwa kuwa wananchi huweza kupata athari za moja kwa moja au kinyume chake kutokana na sera za afya ya jamii na mikakati iliyopo; ipo haja yakuhakikisha ushiriki wao unakuwa madhubuti, huru na wenye maana katika kuweka vipaumbele, kufanya maamuzi, kuandaa mipango, kutekeleza na kuchambua mara kwa mara mikakati hiyo ili kupata huduma bora za afya. Hivyo basi, katiba inapaswa iwawezeshe wananchi (kama wamiliki halali wa haki) kuwa na uwezo wa kisheria wa kuiwajibisha serikali (kama mtoa huduma) kwa hatua inazochukua na isizochukua katika ngazi ya jamii na taifa. Bila kuwa na msingikama huu, mfumo wa afya utabaki kuwa katika hatari ya kutofikia mahitaji ya wananchi.

Katika rasimu ya katiba mpya, ibara ya 46 (1) inaitaka serikali kutoa muongozo wa kisheria unaoruhusu wananchi kushiriki katika kufanya maamuzi ya kijamii yahasuyo afya. Hata hivyo, ili kufanikisha ushiriki wa wananchi kikamilifu, ni muhimu kuhakikisha kuwepo kwa haki yao ya kutafuta, kupokea na kubadilishana taarifa zinazohusu afya.

46. - (1) Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha makundi madogo katika jamii:

- (a) Kushiriki katika uongozi wa mamlaka za nchi;
 - (b) Yanapewa fursa maalum za elimu na fursa za kujiendeleza kiuchumi na fursa za ajira; na
 - (c) Kutengewa maeneo ya ardhi ambayo kwa desturi makundi hayo kuitumia kama eneo la kuishi na kupata riziki ya chakula.
- (2) Serikali na mamlaka za nchi zitachukua fursa za makusudi za kukuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kuweka miundombinu ya makazi, elimu na afya kwa ajili ya kizazi cha sasa na vijavyo vya jamii ya watu walio katika makundi madogo.

Ibara ya 46 (2) inaipa jukumu serikali la kutengeneza miundombinu ya makazi, elimu na afya. Kulingana na ibara hii, mahakama yoyote itakayopaswa kuamua kama ibara hii imekiukwa itakuwa na wakati mgumu wa kutambua kama kiasi, upatikanaji, ukubalikaji au ubora wa miundombinu unajitosheleza au la. Kwa sababu hiyo, ni muhimu kujumuisha vigezo hivyo vya ziada katika sheria mama. Ukiachana na miundombinu tajwa, ukuzaji wa ustawi wa wananchi pia huhitaji vipengele muhimu kama watoa huduma za afya waliofuzu, vifaa tiba hai na upatikanaji wa dawa muhimu.

HAKI YA AFYA NDANI YA KATIBA MPYA

NINI MAANA YA 'AFYA'?

Ili kuwa na huduma bora za afya katika jamii ya Tanzania, katiba ijayo inapaswa kuwa na muongozo unaoweka haki ya afya kwa wote, na kutoa muongozo ni namna gani haki hizo zinaweza kupatikana. Hatua ya kwanza ni kutoa maana ya kina ya haki ya afya. Kwa kuzingatia maana inayotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO).¹² tunakubaliana na mtazamo wa kuwa afya ni “hali ya kuwa na uzima wa mwili, akili na kijamii na si tu hali ya kutokuwa na magonjwa au maradhi.”¹³

NINI VIASHIRIA VYA AFYA?

Haki ya afya haipaswi kufungwa tu kwenye huduma za afya. Watu wanapaswa kuwa na uwezo wa kufurahia maisha yenye afya njema. Hii inapaswa kujumuisha viashiria vya afya kama lishe bora, maji safi na salama, malazi bora na safi, mazingira salama ya kufanyia kazi, mazingira salama, upatikanaji wa elimu na taarifa kuhusu afya na fursa ya kushiriki katika kufanya maamuzi yanayoathiri maisha na afya za watu.

Kutokana na sababu tajwa hapo juu, tunapendekeza tafsiri ifuatayo ya Haki ya Afya ijumuishwe kwenye katiba mpya.

- (1) *Kila mtu ana haki ya kufurahia kiwango cha juu kinachofikika cha afya ya mwili na akili na uboreshaji toshelezi wa hali ya maisha ikijumuisha:*
 - (a) *Afya muhimu ya msingi,*
 - (b) *Malazi bora,*
 - (c) *Maji safi na salama,*
 - (d) *Chakula cha kutosha,*
 - (e) *Mazingira salama,*
 - (f) *Mazingira salama ya kufanyia kazi,*
 - (g) *Ulinziwa jamii katika mazingira ambapo jamii yenyewe haina uwezo wa kujilinda*
 - (h) *Upatikanaji wa elimu na taarifa zihusuzo afya, na*
 - (i) *Ushiriki katika kufanya maamuzi ya kisiasa katika masuala ya afya katika ngazi ya jamii na taifa.*

¹² World Health Organization.

¹³ World Health Organization (2006), Constitution of the World Health Organization, preamble.

HAKI YA AFYA KWA KILA MTU

Ibara tajwa hapo juu inahakikisha kuwa kila mtu anapata haki ya huduma ya afya na viashiria vya afya bila ubaguzi wa rangi, jinsia, lugha, dini, msimamo wa kisiasa au mtizamo mwingine, wa kitaifa au kijamii, mali, asili, udhaifu wa mwili au akili, hali ya afya (ikijumuisha VVU/UKIMWI) na uraia, siasa, msimamo wa kijamii au mwingine wowote, wenye madhara au lengo la kuzuia mtu kufurahia haki sawa ya afya.

HAKI YA KUWA NA AFYA

Ufurahiaji wa afya na hali nyingine muhimu bado ni changamoto kubwa kwa Tanzania kwani nchi inakumbwa na mzigo mkubwa wa magonjwa huku kukiwa na uhaba wa rasilimali. Hali hiyo inasababishaserikali kushindwa kuhakikisha upatikanaji wa afya bora kwa kila mtu. Haki ya kufurahia kiwango cha juu kinachofikika cha huduma ya afya inahusiana na hali ya asili na mazingira tofauti ya kijamii na kiuchumi vya kila mtu na serikali ina ukomo wa rasilimali kwa ajili ya kutimiza mahitaji hayo. Kwasababu hiyo, haki ya afya itambulike kama ni haki ya kufurahia wingi wa vituo vya kutolea huduma za afya, vifaa tiba na huduma katika kuboresha maisha ya watu ili waishi maisha yenye afya njema. Hii inaipa serikali wajibu wa kuwa makini katika kuhakikisha kuwa upatikanaji wa afya bora unafikiwa kwa haraka kwa kiwango cha rasilimali zinazopatikana na kwa uchumi wa taifa unaokua.

AFYA YA MSINGI

Kunapokuwa na upungufu wa rasilimali fedha na rasilimali watu, ni muhimu sana kuhakikisha kuwa mikakati iliyopo inalengwa na kutumika ili kupata ufumbuzi. Ushahidi wa kimataifa umeonyesha kuwa mifumo ya afya yenye lengo la kuboresha afya ya msingi ya jamii imekua na matokeo bora zaidi, yenye gharama za chini na kuridhisha kwa watumiaji. Hivyo basi, sheria mama mpya inapaswa kutambua umuhimu wa kutoa afya bora ya msingi.

Kuweka msisitizo katika afya ya msingi, serikali inapaswa kuweka wazi jukumu lake la kutoa huduma sawa za afya katika kinga, tiba na huduma ya kurekebisha afya na elimu ya afya; programuza vipimo za mara kwa mara pamoja na tiba sahihi kwamagonjwa yanayosumbua watu wengi mara kwa mara, magonjwa ya kuambukiza, ajalina ulemavu hasa katika ngazi ya jamii; utoaji wa dawa muhimu; na upatikanaji wa huduma na tiba sahihi ya afya ya akili.

MAJUKUMU YA DOLANI YAPI?

Katika hatua ya pili, sheria mama inapaswa kuchanganua majukumu ambayo serikali inapaswa kutekeleza ili kufikia upatikanaji wa haki zinazotokana na tafsiri ya Haki ya Afya. Haki ya afya inaelezwa kuwa kufurahia haki ya afya kwa watu wote na maisha. Kufurahia mazingira mazuri na afya njema vinaweza kufikiwa endapo tu rasilimali zilizopo zitaendelezwa. Hii hailazimishi serikali kuanza kutimiza wajibu wake kwa jamii kwa kuwa Haki ya afya itaanza kutekelezwa kisheria. Baada ya kupitishwa kwa sheria inayohusiana na masuala ya afya, serikali inapaswa kutunga sera, programu and mipango kazi inayolenga kutekelezwa ndani ya muda fulani.

Ili kuweza kufurahia Haki ya Afya, serikali inapaswa kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa kiasi cha kutosha wa vituo vya kutolea huduma ya afya, vifaa tiba na huduma ambavyo ni mahitaji muhimu ya

¹⁴ Director-General of WHO, Dr. Margaret Chan, (2007) at the International Seminar on Primary Health Care in Rural China.

¹⁵ Declaration of Alma-Ata (1978).

¹⁶ United Nations Committee on Economic, Social and Cultural Rights (2000), General Comment No. 14, uk. 4f.

afya ya msingi na tiba ya mambo mengine muhimu yanayosababisha mtu kuwa na afya bora kama maji safi na salama. Zaidi ya hayo, huduma zote za afya na mahitaji yahasuyoyafya yanapaswa kupatikana na kufikiwa kwa urahisi hasa namakundi yenye mahitaji maalum kama watoto, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na wagonjwa wa akili. Serikali pia inatakiwakuhakikisha kuwa vituo vyote vya tiba, vifaa tiba na huduma zitolewazo ziko katika kiwango kinachotakiwa katika maadili ya fani ya tiba, yenye kuzingatia jinsia na umri, na yenye kuboresha hali ya afya ya wagonjwa. Ubora unataka vituo kutoa tiba kwa kutumia vifaa vya kutosha, kuzingatia usafi na kuwa na watoa huduma wenye ujuzi wa kutosha wanaoweza kutoa dawa zinazotibu na zisizoharibika.

Kutokana na sababu tajwa hapo juu, tunapendekeza kuwa majukumu yafuatayo yajumuishwe kwenye katiba mpyana serikali iyatimize.

(2) Ni jukumu la serikali kuchukua hatuasahihi za kisheria na nyingine, zilizo ndani ya rasilimali zilizopo, kuhakikisha uwepo, upatikanaji, ubora wa vituo vya tiba unaokubalika, vifaa tiba na huduma zenye ubora hasa kwa makundi maalum na makundi yaliyo katika mazingira magumu kama vile wanawake, watoto, wazee, watu wenye ulemavu na wagonjwa wa akili.

DHARURA ZA KIAFYA

Mfumo wa afya wa taifa umegawanyika katika ngazi saba. 1. Huduma ya afya ya kijiji, 2. Zahanati, 3. Vituo vya afya, 4. Hospitali za wilaya, 5. Hospitali za mkoa, 6. Hospitali za Rufaa, 7. Matibabu nje ya nchi. Kila ngazi ya kituo inaweza kumpa mgonjwa rufaa kwenda kwenye kituo cha juu zaidi ili kumpatia mgonjwa matibabu yenye utaalumu na vifaa vya hali ya juu zaidi.

Hata hivyo, inapotokea dharura, kituo chochote cha tiba kinapaswa kuwapatia wagonjwa huduma ya dharura ili mradi rasilimali zinazohitajika zinapatikana kituoni hapo. Hii inamaanisha kuwa, vituo binafsi vya tiba vinapaswa kutoa huduma ya dharura kwa mgonjwa yeyote anayehitaji huduma ya dharura hata kama mgonjwa hana uwezo wa kulipia gharama hizo. Na ni baada ya kutuliza maumivuya ugonjwa ndipo mgonjwa anaweza kuhamishiwa kwenye kituo kingine.

Kutokana na sababu tajwa hapo juu, tunapendekeza haki ifuatayo itolewe kwa tiba ya dharura na ijumuishwe kwenye katiba mpya.

(3) Hakuna mtu yeyote atakayezuiliwa kupata huduma ya tiba ya dharura.

MAONI YAKO NI YAPI?

Hadi sasa, haki ya afya haipo kati ya haki zinazoweza kudaiwa nchini Tanzania. Maandalizi na utekelezaji wa katiba mpya yanawapa watanzania nafasi ya kihistoria ya kuondoa hali hii isiyokubalika. Tunakuaribisha kutoa maoni yako kuhusu maswala yaliyoelezwa ndani ya taarifa hii na maoni mengine yoyote.

twitter: @sikika1

Tovuti: www.sikika.or.tz

Barua pepe: info@sikika.or.tz

Sikika inafanya kazi
kuhakikisha usawa katika
upatikanaji wa huduma bora
za afya, kwa kutathimini
mifumo ya uwajibikaji katika
ngazi zote za serikali.



Nyumba Na.69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183
Dar es Salaam, Tanzania.

Simu: +255 22 26 663 55/57
Ujumbe mfupi: 0688 493 882
Faksi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania.
Simu: 0262321307
Faksi: 0262321316